MTANIJENGEA NYUMBA GANI?

Asante, Ndugu Green. Ni majaliwa. Salamu kwa Ndugu na Dada Green, na wote waliopo hapa asubuhi ya leo. Na ni majaliwa ambayo ninajisikia nimejipa, kuja mahali hapa pa kuabudia, kufanya matangazo machache.

2 Sitaki kuuchukua wakati wa Ndugu Green hapa, kwa kuwa nimemsikiliza Ndugu Green mara kadhaa, akihubiri, na bila shaka nilishawishika, na wakati akituletea Neno la Bwana, na ni mnyenyekevu sana kulihusu. Jana yeye alisema, "Sipati Neno toka kwa Bwana jinsi ambavyo labda lingekuja kwa ufunuo, ji—jinsi limetumwa, bali," kasema, "ninapenda ku—kutia mkazo kwa yale ambayo yamesemwa." Akasema, "Kama vile Paulo alipoandika jambo fulani katika Biblia, naja hapa kutilia mkazo yale aliyosema." Kasema, "Sina ujumbe wowote, ni kutilia mkazo tu yale ambayo yamesemwa tayari kutoka kwa Bwana." Sasa hilo lilikuwa halina kifani kweli, ja—jamaa mdogo namna hiyo, na kusema, kutoa tamshi kama hilo.

Sasa hebu na tuombe tu pamoja.

3 Mungu mpendwa, ni vigumu kwangu kujua jinsi ya kuanza, kwa kuwa ninajisikia Wewe upo hapa leo, na katika Uwepo Wako daima tunajisikia duni sana. Nami na—nakushukuru kwa majaliwa haya. Sasa, Bwana, kwamba umetukabidhi mahali hapa, tunaomba ya kwamba utakutana nasi kila wakati tunapokutana hapa. Na jalia Roho Wako Mkuu atende kazi kwenye jiji hili! Jalia tuweze kuuleta Ujumbe huu wa Injili ambao tumepewa na kukabidhiwa mikononi mwetu katika siku hizi za mwisho, jalia utimizwe, Nawe umpate kila nafsi kutoka Tucson na vitongoji vyake, ambaye Wewe ulimkusudia apate Uzima. Tujalie mambo haya, Baba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

4 Nafikiri ninataka kusoma kifungu kidogo cha Maandiko hapa asubuhi hii, kabla tu sijasema maneno haya ninayotaka kusema. Yanapatikana katika Matendo, mlango wa 7 wa Kitabu cha Matendo. Na wakati mkifungua hapo, tutaanzia kwenye kifungu cha 44.

5 Sasa tutaenda Shreveport juma hili, juma hili lijalo, kwa mfululizo wa ibada, na sasa tutajaribu, Bwana akipenda. Ndugu Moore, Ndugu Jack Moore, rafiki msiri sana wangu mimi pamoja na Ndugu Pearry, nasi tunampenda Ndugu Jack. Ujumbe, nafikiri, kwa namna fulani ulimshangaza kidogo, hasa sana juu ya baadhi ya mambo ambayo tunayathamini sana na kuyaamini, ambayo—ambayo yalitujia kwa kule kufunguliwa kwa Mihuri Saba, tunavyoiamini, kama vile, "uzao wa nyoka," na "Usalama wa milele wa waaminio," na—na kadhalika, baadhi ya Jumbe

hizo. Hizo, labda kwa wengine. . .Hatufikirii kwamba Huu ni mgumu, bali, Huu, inakubidi kuufungua moyo wako kwenye Kweli. Tunaamini ya kwamba tunaishi katika wa—wakati wa mwisho. Hilo ni dhahiri sana kwetu, ya kwamba tuko tu kwenye mwisho wa safari.

6 Na kuhubiri katika kanisa la mtu mwingine, vema, unataka kuuheshimu ukarimu wa mtu huyo, wa—wa kukupa nafasi hiyo ya kuja kanisani mwake. Nami, hakika, nikijua ya kwamba wao hawauamini Huo, nami ningewaheshimu vya kutosha hata. . .Kuna mengi zaidi ninayoweza kuhubiri huko, mbali na kuuingiza Huo ndani; isipokuwa iwe ni Roho Mtakatifu anausukuma Huo kidogo, mnaona, basi bila shaka ningesema kama alivyosema Yeye. Wala sijui lingine ila kufanya hivyo, nami natumaini kamwe sitajifunza vema zaidi ya kufanya hivyo. Mnaona? Hebu na tuliseme tu jinsi Yeye anavyolisema.

7 Sasa hebu tusome ki—kifungu kimoja tu ama viwili hapa kutoka kwenye m—mlango wa 7 wa Kitabu cha Matendo, kuanzia kifungu cha 44.

> *Ile hema ya ushahidi ilikuwa pamoja na baba zetu jangwani, kama alivyoagiza yeye aliyesema na Musa, ya kwamba aifanye sawasawa na mfano ule aliouona;*
>
> *Ambayo baba zetu, kwa kupokezana, wakaiingiza pamoja na Yesu katika milki ya Mataifa wale, ambao Mungu aliwafukuza mbele ya baba zetu, mpaka siku za Daudi;*
>
> *Aliyepata fadhili mbele za Mungu, naye aliomba ampatie Mungu wa Yakobo maskani.*
>
> *Lakini Sulemani alimjengea nyumba.*
>
> *Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, kama vile asemavyo nabii,*
>
> *Mbingu ni kiti changu cha enzi,. . .nchi ni pa kuwekea miguu yangu; ni nyumba gani mtakayonijengea? Asema Bwana, au ni mahali gani nitakapostarehe?*
>
> *Si* mikono yangu iliyofanya *haya yote?*

8 Juu ya Huku, kusomwa kwa Maandiko haya, ninataka kusema maneno machache ninayotaka kusema kabla Ndugu Peary hajauleta ujumbe wa asubuhi.

9 Ninaona huu ni mmoja wa nyakati kuu sana za kuzuru kwangu Tucson. Nilikuja hapa kwa sababu niliongozwa kuja hapa. Nilikuja hapa kwa kuwa Roho Mtakatifu, kupitia ono, alinituma hapa. Ninajua hilo linaweza likaonekana lisilo kawaida, labda. Lakini Yeye, kadri nijuavyo mimi, jambo lolote ninalojua juu ya Mungu, nilitumwa Tucson kwa ono. Nimeshangaa jinsi nilivyopata kutumwa mahali hapa pa jangwa. Na halafu hapa ambapo pana. . .

10 Tukinena kiroho, juu ya jiji hili, sijui mahali popote ambapo pamekufa kiroho zaidi, kuliko jiji la Tucson. Vipo vita baina ya makanisa. Kuna mizozo baina ya makusanyiko. Hamna umoja, na kila mtu ananyakua, na kushikilia, na kufinya, na kujaribu kumpata *huyu*, na kumshawishi abadili imani. Ni jangwa, tukinena kiroho, pia.

11 Lakini hata hivyo nilisoma katika Biblia, ambapo Mungu alimwita Musa awaache wapendwa wake na yote aliyopenda, na kumtuma nyikani, apate kuziandika Torati za Biblia. Hilo lilikuwa ni Agano la Kale, vile Vitabu vinne vya kwanza, Mwanzo, Mambo ya Walawi, na Kumbukumbu la Torati, Kutoka. Yeye. . .Kamwe sikuvitaja jinsi vinavyofuatana, bali hivyo ni Vitabu vinne. Hivyo kweli ndivyo Agano la Kale. Kwa sababu, hivyo vilivyobakia vilikuwa ni yale waliyosema manabii, katika Zaburi za Daudi, na kadhalika, bali Mambo ya Nyakati ya wafalme. Bali hivyo vilikuwa ndivyo misingi na kanuni za Agano la Kale. Musa ndiye aliyeviandika baada ya kuitwa atoke kwenye nchi ya uenyeji wake, ambako alizaliwa na kukuzwa miongoni mwa watu wake, naye akatumwa jangwani, kuandika Kitabu hiki cha Agano la Kale.

12 Ndipo ninaona ya kwamba katika Kitabu cha Agano Jipya, ambapo Paulo, ambaye ndiye mwandishi wake, ama si mwandishi, bali ndiye aliyeliandika Agano Jipya. Pia yeye aliondolewa miongoni mwa watu wake, na, kwa Roho, akaenda Uarabuni, ambako alikuwa kwa muda wa miaka mitatu na nusu, apate uvuvio. Naye Paulo ndiye mwandishi mkuu wa Agano Jipya. Sasa, wapo Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, bali walikuwa ni waandishi walioandika tu yale Yesu aliyosema huku wakimfuatilia. Na, lakini, ukikichukua Kitabu cha Timotheo, na kwa Warumi, na kwa Waebrania, na kadhalika, Paulo alipokea uvuvio kuliandika Agano Jipya; akilichukua Agano lote la Kale kama kivuli, na kuliweka katika utaratibu. Naye Mungu akaheshimu jambo hilo, na kulifanya Agano Jipya.

13 Na sasa ikiwa ilibidi Agano la Kale liondolewe kutoka kwa ninii. . .ilibidi mwandishi huyo aondolewe kwa watu wake, aingie nyikani, apate uvuvio wa kuandika Agano la Kale. Na katika Agano Jipya, aliyeliandika aliondolewa na Mwandishi, akapelekwa mahali pa jangwa, apate uvuvio wa kuliandika Agano Jipya. Navyo Vitabu hivyo vimefungwa kwa Mihuri Saba; ingehitaji jambo lilo hilo, ninaamini, katika siku hizi, kuifungua hiyo Mihuri Saba. Kuacha yale unayothamini, yale unayopenda sana, na makazi madogo niliyopewa na watu, na miongoni mwa watu wangu wote na marafiki, na kanisa lililokuwa likisitawi, wala halikupungukiwa na kitu; na ku—kuyaacha hayo, kujiondoa kwake, na kuhama, kuingia katika jangwa ambako hukumjua mtu, na kila kitu kinakupinga.

14 Lakini kuna jambo fulani kumhusu Mungu, ya kwamba Yeye humsukuma mtu kufanya mambo ambayo yamepita mawazo

yake yote, kusudi yawe ni kwa ajili ya utukufu na heshima ya Mungu. Nami ninajisikia ya kwamba, sio kwa kujiheshimu, bali na—naona ilikuwa ni baraka kuacha kila kitu nilichopenda, kuhamia huku kwenye nyika hili na kuteseka jinsi ambavyo sijawahi kuteseka maishani mwangu, hapa kwenye nyika hili, ama jangwa hili. Ila ninaamini, ya kwamba katika kufanya jambo hilo na kutii yale Mungu aliyoamuru yafanywe, Mungu ametufungulia siri za siku hii ya mwisho. Nasi tupo hapa na Ujumbe huu.

15 Sasa, kulikuwa na watu wengi walionifuata, na hilo si jambo lisilo la kawaida. Kwa kawaida mtu tunayeninii . . . Watu wanapendana, nao huo, upendo, utakusukuma kufanya mambo usiyowazia ungeyafanya. Na wengi wenu mliyaacha makazi yenu, mliacha yote, kuenda tu, mkaja huku jangwani.

16 Wengi wamenipigia simu, wengi wameniuliza, "Je! tuje Arizona? Pangekuwa ni mahali pazuri kwetu?" Vema, kama ilivyosemwa juu ya Musa na hao wengine, hapakuwa ni mahali pa tunda, si mahali pa komamanga.

17 Hapa hakuna kazi nyingi za kufanya, na maisha ni magumu, na gharama ya maisha ni kubwa. Kwa kweli ni mahali pagumu pa kuishi, huku Tucson, Arizona; mishahara ni duni, na—na chakula ni ghali, na kodi ya nyumba. Ni—ni mahali pabaya sana pa kuishi, kwa njia hiyo. Bali pana afya nzuri, ni pakavu. Nasi wakati mwingine . . . Haitupasi kufanya nia zetu zifanane na mambo ya dunia hii.

18 Hatuna budi kuutazamia uongozi wa Roho Mtakatifu. Bali jambo moja lililonisumbua katika kuja hapa, na kuwaambia watu, vema, "haiwapasi kuja" ama "mnapaswa kuja," hilo ninamwachia kila mtu binafsi, jinsi Mungu anavyomwongoza mtu huyo kufanya. Nafikiri kila mmoja wetu anapaswa kufanya hivyo, aongozwe na Roho, juu ya jambo la kufanya.

19 Na wengi wenu hapa mmetoka karibu na Jeffersonville, na kusanyiko kule, nanyi mmekuja huku. Sasa, jambo lililonisumbua, lilikuwa ni mahali pa kuabudia.

20 Nami natambua, kama nilivyosoma kwenye Maandiko hapa, juu ya Stefano na hotuba yake kabla tu ya kifo chake; kwa kuwa walimpiga mawe mara baadaye, kwa ajili ya ujumbe wake. Alipokuwa akinena, alisema, "baba zetu," akinena juu ya Waebrania katika siku za mwanzoni, jinsi ambavyo walijaribu kupata kibali mbele za Mungu, kujenga mahali pa kuabudia. Alisema ya kwamba, "Sulemani alimjengea nyumba, ama jengo." Tunaifahamu hadithi hiyo.

21 Bali ninayapenda maneno yake yanayofuata, "Ila Yeye aliye Juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono," na mahali pengine katika Isaya. Yeye alisema, "'Umeniandalia mwili; unaona, dhabihu na sadaka, na mijengo, na kadhalika, bali umeniandalia Mimi mwili.'" Vema, tunatambua ya kwamba

wakati huo alikuwa akinena juu ya mwili ambamo Mungu aliishi, katika Kristo.

22 Lakini ninaamini siku hizi, ya kwamba uvuvio ambao umemjia nanii—Ndugu Green, kuhamia hapa, yeye na Dada Green, wakayaacha makazi yao huko mashariki, tena, pia, huko Texas, kuja hapa pamoja na. . .kuanza bila kitu; kwa uvuvio tu, wakijisikia ya kwamba wanapaswa kufanya hivyo. Ninawathamini watu watakaoufuata mwongozo wa Kristo, haidhuru gharama itakayowagharimu.

23 Ingawa ulimwengu wote, labda marafiki wako walio wazuri kuliko wote, wanadhani kwamba umekosea, bali kwako si kosa. Mradi tu unajisikia ya kwamba kuna jambo fulani nyuma yake, ni Mungu anayekuongoza; kamwe haikosei, na daima itatokea vizuri.

24 Watazameni hawa mume na mke vijana, kijana mwanamume mwenye kipaji. Sisemi jambo hili kwa sababu ameketi hapa. Na mama huyu mdogo pamoja na watoto wake wachanga, akiwa na familia ya kulea, naye ameiacha kazi yake na kila kitu, kuja hapa.

25 Ninatambua ya kwamba miaka kadhaa iliyopita niliitwa hudumani. Kamwe sijawahi kuwa mchungaji aliyefanikiwa, kwa sababu nina roho ya kutangatanga, na kurandaranda. Siwezi kuridhika mahali popote. Popote tu Roho aendako, sina budi tu kuambatana Naye, kwa kuwa mimi nina Ujumbe. Yesu alisema, "Sina budi kuhubiri katika mji huu mwingine pia."

26 Bali wapo wale ambao ni wachungaji wanaolichunga kundi. Ninashukuru sana ya kwamba Ndugu Pearry aliufuata uongozi wa Roho Mtakatifu, na leo hii tuna maskani. Ni ndogo. Hiyo ni nzuri kutosha ya kianzio, kuona kile Roho Mtakatifu. . .Bila kujua, hebu twenende tu hatua kwa hatua. Sasa, ninaamini, kama Mungu amenena na Ndugu na Dada Green, kuja hapa, na amefungua mahali ambapo watoto wetu; badala ya kuendesha baisikeli zao Jumapili asubuhi, na mitaani na wakizurura-zurura, wana mahali pa kuja kuabudia, badala ya kuketi kitako na kusikiliza jambo fulani ambalo tumesikia kwenye redio, ambalo ni sawa.

27 Lakini sisi, kama kundi hili la watu, tunao Ujumbe kwa ajili ya siku hii. Sisi, tunaamini ya kwamba Mungu ametupa Ujumbe. Naye Ndugu Green, ni, sitaki kumwita mwenzangu, kwa sababu sisi tunaninii. . .Vema, ndivyo alivyo, pia, mwenzangu, tuko pamoja katika Ujumbe huu. Ndugu Green huhubiri jambo lile lile pamoja na Ujumbe ninaoamini. Ameyaacha makazi yake, amewaacha watu wake, ameliacha kanisa lake. Alikuwa, ninaamini, alikuwa mkuu wa jimbo ama kitu kama hicho, wa moja ya mashirika hayo, naye akakiacha kitu hicho chote alipousikia Huu. Aliacha kila kitu alichothamini, pia, aje jangwani, kusaidia tu kile Mungu anachotupatia sasa.

28 Ninasema si kwamba tu anapaswa kuwa mioyoni mwetu, inapaswa kuwa ni jukumu letu kumuunga mkono, kila tuwezacho, kuzihudhuria ibada, kuja hapa kuabudu, na kupafanya mahali hapa kuwa mahali ambapo Mungu anaweza kutufunulia mambo aliyo nayo ya kutufunulia. Na kama neno Lake lilivyosema, "Ujumbe haunijii mimi kwa kutolewa kwa uvuvio, kama unavyofanya kwa labda baadhi yetu, lakini," yeye alisema, "Nipo hapa kuunga mkono kile Mungu ametoa." Ni tamshi la jinsi gani! Nami ninaamini, kama sote tutashirikiana pamoja, tutaiweka mioyo yetu kwa hilo.

29 Ninajua ya kwamba kila mmoja wenu, kama mnajisikia jinsi ninavyojisikia, nina njaa sana ya kumwona Roho wa Mungu akitenda kazi, ni vigumu kwangu kustahimili hilo. Matukio fulani ambayo ndiyo kwanza niyapate huko mlimani, kujisikia tu ya kwamba mara nyingine tena, kile kitu Fulani ambacho wakati nilipookoka kwa mara ya kwanza kilikuwa ni cha ajabu sana moyoni mwangu! Nasi tunaweza kufikia mahali, tunaweza kuketi na kukiona miongoni mwetu, ya kwamba tunakufa. Tunapoketi hapa jangwani, ninaingia miongoni mwa ndungu zangu, wananizungumzia nami ninawazungumzia; daima, katika njia ndogo ya kuangalia, kuhisi huko nje kwa Roho, tuseme, kuona tu hali ya ndugu huyo, kuona kuna shida gani. Ninaanza kuhisi sisi sote tukitandawaa, tukimwacha Roho. Limekuwa ni jambo la kawaida sana kwetu. Hatuna budi kuabudu katika Roho, ambapo Roho wa Mungu. . . Si kwamba tu Ujumbe wetu unapaswa kuwa ndio mwale wa wakati huu, unapaswa kuwa ndio mwale mioyoni mwetu. Mnaona? Hauna budi kuwa mioyoni mwetu, la sivyo hatuwezi—hatuwezi kuukabidhi vema kwa watu. Roho hana budi kuubeba Ujumbe huu, Yeye Mwenyewe. Nami ninatumaini na kuamini katika kila mmoja wenu, kuwa ni Mkristo halisi.

30 Sasa wanahitaji waalimu wa Shule ya Jumapili. Watahitaji watumishi. Nami ninataka kusema jambo hili ili kwamba mfahamu kabisa. Hili ndilo kanisa langu.

31 Nimekuwa hapa miaka mitatu. Nami nimekuwa na mlango mmoja uliofunguliwa kwangu, huo ulikuwa ni Ndugu Mack aliyeniomba nije nihubiri. Mungu ambariki. Sijaalikwa na watu wengine wowote; sina kitu dhidi yao, wao ni sawa. Ndugu Brock, rafiki yangu mzuri, Ndugu Gilmore, wengi wa hawa ndugu wa Kipentekoste hapa, ni marafiki wangu wasiri sana, sana. Ninawapenda; sina kitu dhidi yao. Ninaelewa hali yao. Hawawezi kunialika mle ndani, kisha wabaki katika dhehebu lao. Mnaona, hawawezi kufanya hivyo. Kwa sababu, wakinialika, wanafukuzwa. Kwa hiyo mnaiona hali yao. Ilinibidi kukabili jambo lilo hilo. Lakini, jamani, daima na iwe, "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu," mapenzi ya Mungu.

32 Na sasa kwa kuwa, Ndugu Green, Mungu amemtuma humu na kutufungulia kanisa la Imani iliyo na thamani kama ile

tunayoamini, inatupasa kuwa na shukrani sana kwa Mungu, na kuhudhuria kila ibada, tuchukue kila mahali tuwezapo. Na kama tukiombwa kuita, kuomba, kutafuta, kufanya, hebu na tuwe askari moja kwa moja kwenye . . . wenye hamu tu ya kulitekeleza. Mnaona?

33 Udumisheni Ujumbe kwa heshima, na muishi maisha yanayostahili. Msiache uchafu wowote uje juu Yake. Tunaishi ambapo wakati umeenda sana sasa. Tume—tumechelewa sana kwenye majira. Hebu tuishi yaliyo safi. Vema, maisha yangu, maisha yako, maisha yetu yote yanapaswa kunyanyuliwa, mbele za Mungu.

34 Vijana wetu wanaendesha kila mahali, kutoka mahali hadi pengine, kutoka kwenye tamasha moja hadi nyingine, wakizidi kuelea mbali na mbali zaidi na Mungu. Kweli. Sasa, hiyo ni kweli. Ninaona jambo hilo katika watoto wangu, nami ninajiona nikififikia mahali ambapo hakuna . . . Ninyi, inawabidi tukutane pamoja, kumwabudu Mungu; Biblia ilisema hivyo, "Tunapoiona siku hii ikikaribia, zaidi sana tuje pamoja." Kama kuna watu wawili pekee hapa, wewe kuwa ni mmoja wao. Sasa hiyo ni . . . Na kama tukikutanika pamoja na kuabudu pamoja, basi tunaninii tu, jambo fulani kulihusu, Yesu alisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, Nipo papo hapo katikati yao."

35 Sasa, kama nilivyosema hapo awali, Ndugu Green aliniambia, naye akalisema. Mke wangu alikuja, akaniambia yale aliyosema nilipokuwa nimeondoka. Kwamba, naye alisema asubuhi ya leo, "Mimbara ilikuwa wazi wakati wowote." Sasa kwa kawaida . . . Hiyo ni, imefunguliwa kwa ajili ya mimi kuhubiri.

36 Sasa, kwa kawaida, ilinibidi kuendesha gari kote mpaka Jeffersonville, Indiana, kuutoa Ujumbe ambao Mungu alinipa, kuwaletea watu; kwenda kote mpaka Jeffersonville, Indiana, na kila mmoja wenu akijiunganisha kote nchini, na kujiunganisha kwa simu na kadhalika, kuupata Ujumbe, kwa sababu huo ndio tunaoishia. Mnaona, hilo ndilo lililotuleta hapa. Vema, haitubidi kufanya hivyo tena.

37 Mungu akinipa Ujumbe, ninaweza kuja papa hapa mimbarani na kuuhubiri, na kujisikia huru kufanya hivyo. Naam. Nami ninaamini, kwa jambo hilo, kwamba Mungu Mwenyezi atawabariki kama tu mtasimama pamoja na kanisa hili sasa, kundi hili la watu. Si hivyo tu, bali hebu tutoke nje tuone kama hatuwezi kuwaleta wengine. Mnaona, hebu tuzungumze na wengine kila mahali, tuzungumze nao kuhusu kanisa letu na linayomaanisha. Yale kanisa letu . . . Tupo hapa. Tunawatakeni mje, mkawalete wageni, nami nina hakika itakuwa ni kwa manufaa yetu sisi sote. Mnaona? Tunalo jengo,

ambalo tunalitolea shukrani. Tunashukuru kwa ajili ya mahali hapa, kukusanyika pamoja.

38 Lakini, "Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, mnaona, 'Kwa kuwa Mbingu ni kiti Changu cha enzi, na nchi ni pa kuwekea miguu Yangu; na ni mahali gani nitakapostarehe? Bali umeniandalia mwili.'"

39 Nasi ni Mwili wa Kristo. Kwa hiyo tunapotoka kwenye jengo moja hadi jengo lingine, ninaamini, katika kuzileta Jumbe zetu, nasi tutashuka tuje na kufanya ibada za uponyaji. Na jambo lolote Bwana atakalotufunulia kufanya, tutakuwa nalo papa hapa kanisani, hata litaongezeka kuwa kubwa mno itawalazimu kulipeleka mahali pengine, na mahali pengine, mpaka Yesu atakapokuja. Mungu awabariki.

40 [Ndugu Pearry Green anatoa mawazo yake, kisha anamwomba Ndugu Branham kumweka wakfu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu.

41 Mungu mpendwa, tunaposimama hapa kwenye jukwaa hili, ambalo linawakilisha, moja kwa moja hapa madhabahuni, tunatambua ya kwamba sisi ni ja—jamii ya watu wanaokufa, kuhusu mambo ya dunia hii. Tunaangalia huko nje mitaani na kuona dhambi imeandikwa kila mahali, na kwamba Utukufu wa Bwana unaondoka upesi. Nasi tunajua, wakati Utukufu wa Bwana utakapopaa juu, nalo Kanisa litaenda pamoja Nao. Mungu, tunataka kuwa kule.

42 Siku chache tu zilizopita, nikisimama hapa pembeni mwa barabara, ng'ambo tu ya barabara, nikiangalia lile gwaride likishuka kwenda barabarani; na nikiviona hivyo vifaru vya kale vya Vita Vya Kwanza vikiongoza, ndipo kikaja kifaru kikubwa na kizito cha Sherman, nyuma ya hicho vikafuata na kufuatana, kisha akina mama wenye nyota za dhahabu; maskini familia ndogo iliyovunjika, huku mke analia, na maskini mvulana mdogo mwenye matambara aliyempoteza baba yake, maskini mama kizee alikuwa amempoteza mwanawe. Nikawazia, "Ni huzuni jinsi gani," kusimama pembeni mwa barabara na kuangalia kitu kama hicho kikipita. Kisha kuona, mara tu walipolipita jengo hili, muziki ukabadilika ukawa, *Twendeni, Askari Wakristo*. Wakipiga hatua zao taratibu, nyuma; bali walipopita mahali hapa!

43 Mungu mpendwa, ninawazia juu ya wakati mwingine mkuu unaokuja, na huo utakuwa ni ule ufufuo, wakati watu wa zamani watakapofufuka kwanza, watakatifu, wale wazee. "Kwa maana sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia wale waliokwisha kulala mauti; kwa sababu parapanda ya Mungu italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza." Ndipo tutakapoona hiyo ninii kuu. . .watu tu wakienda, wakitembea taratibu kupitia angani; nasi tutakuwa

tumesimama, tukikungojea kubadilishwa kwetu, tukijua ya kwamba tutaingia mstarini, pia. Mungu, tufanye askari waaminifu.

44 Ni wale tu ambao kweli wamehusika na wamekuwa vitani wangejua kile hilo linamaanisha hasa, kuviona vifaru hivyo vikifingirikia hapo. Na, Mungu, tunafikiri ya kwamba wale ambao wamekuwa katika vita vya uzima watajua maana yake, wakati tukingojea nafasi yetu kuingia mstarini na mahali petu, katika ule ufufuo, kupaa juu.

45 Na huyu, ndugu yangu mdogo, anayesimama hapa, amefunzwa vizuri, yuko tayari, amevaa nguo, akimngojea mzee kumwekea mikono, mzee shujaa anayetoka pale kwenye mstari wa mbele wa vita, akijua ya kwamba hana budi kuingia vitani, pia. Mungu mpendwa, kwa mikono hii isiyostahili niliyoiweka juu ya ndugu yangu, ikiiwakilisha Yako. Mbariki Ndugu Green, Mungu mpendwa, ambaye ninambariki katika Jina la Yesu. Jalia aubebe Ujumbe huu, Bwana, katika jiji hili na popote utakapomwita. Jalia awe mwaminifu, amejazwa na Roho, akiishi maisha yasiyo na lawama. Mungu, jalia aihurumie mioyo ya watu, apate kuwafundisha na kuwaongoza na kuwaelekeza kwenye njia ambayo sote tunatamani kuipitia. Tujalie, Bwana.

46 Mbariki mke wake mwaminifu, watoto wake wadogo. Bariki jitihada zetu hapa pamoja, kama ndugu Wakristo hapa duniani, tupate kuipeleka Injili hii hata miisho ya ulimwengu. Mtume Roho Wako juu yake, Mungu. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo, tunapomkabidhi Kwako. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu Pearry. Libebe Neno la Mungu!

Mtanijengea Nyumba Gani? SWA65-1121
(What House Will You Build Me?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 21 Novemba, 1965, kwenye Maskani ya Tucson huko Tucson, Arizona, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org